**RISALA YA UTII KWA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN; RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KUTOKA KWA WANANCHI WA WILAYA YA SUMBAWANGA WAKATI WA MBIO MAALUM ZA MWENGE WA UHURU LEO TAREHE 20/09/2021**

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Rais,** Sisi Wananchi wa Wilaya ya Sumbawanga, kwa heshima na taadhima tunayo furaha kubwa kuupokea na kuukimbiza Mwenge wa Uhuru Mwaka, 2021. Wilaya yetu ina Tarafa 6, Kata 46, Vijiji 138, Mitaa 165 na Vitongoji 667. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, Wilaya ilikuwa na jumla ya watu 515,639 ambapo Wanaume ni 249,796 na Wanawake ni 265,843. Kutokana na ongezeko la asilimia 3.2 kwa sasa Wilaya inakadiliwa kuwa na jumla ya Watu 653,339 ambapo Wanaume ni 318,761 na Wanawake ni 334,578. Tunatambua kuwa, Mwenge wa Uhuru ni ishara ya kuleta Upendo, Utulivu, Amani na Mshikamano miongoni mwa Watanzania katika kusukuma shughuli za maendeleo ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi.

## 2.0 UJUMBE WA MWENGE

**Mheshimiwa Rais,** Mwenge wa Uhuru wa Mwaka 2021 umebeba ujumbe Mkuu usemao'***'TEHAMA ni msingi wa Taifa endelevu; Itumie kwa usahihi na Uwajibikaji***". Ujumbe huu unalenga kuhimiza umuhimu wa matumizi ya TEHAMA kwa maendeleo ya Watu kwani, kwa sasa matumizi ya TEHAMA kwa Wananchi yameongezeka katika nyanja mbalimbali za Kijamii Kilimo na ufugaji, Viwanda, Biashara, Afya na Elimu. Ongezeko la matumizi haya ya TEHAMA yamesaidia kwa kiasi kikubwa ongezeko la Uchumi na Ustawi wa Jamii kwani imerahisisha shughuli zao za kila siku. Pamoja na mafanikio hayo ya TEHAMA Wilaya imeendelea kusisitiza juu ya Matumizi sahihi ya TEHAMA. Hivyo Wananchi wanawajibu wa kufuata kwa usahihi matumizi ya TEHAMA kwa kufuata kanuni, Sheria na Taratibu. Hivyo Wananchi wanawajibika kutambua matumizi sahihi ya TEHAMA ikiwa pamoja na utunzaji wa miundombinu yake.

### 2.1 Matumizi Sahihi ya TEHAMA katika Uwajibikaji

**Mheshimiwa Rais, Matumizi** ya TEHAMA yamerahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi kwa mfano katika sekta ya Afya matumizi ya mfumo wa Got-Homis ambapo umepunguza muda katika utoaji wa huduma kwa wateja. Pia kwa kutumia mfumo wa LGRCIS umesaidia ongezeko la makusanyo ya Serikali kutoka shillingi 2,551,154,685.88 Mwaka 2015/16 hadi shillingi 5,100,219,059 Mwaka 2020/21 sawa na ongezeko la asimila 50%. Sambamba na hilo matumizi ya mfumo wa TEHAMA yameongeza udhibiti wa matumizi ya fedha katika Taasisi Binafsi na Serikali kama vile mashuleni, Maeneo ya kutolea huduma za Afya.

Mheshimiwa Rais, Pamoja na Ujumbe Mkuu wa Mwenge Maalum wa Uhuru wa Mwaka, 2021 umeambatana na kaulimbiu zingine 5 kama ifuatavyo: -

### 2.1.1 Mapambano dhidi ya Rushwa

**Mheshimiwa Rais**, kwa kutambua kuwa mapambano dhidi ya rushwa si ya Serikali pekee bali ni ya kila mmoja wetu tunaunga mkono kwa dhati Ujumbe wa Mwenge wa uhuru wa Mapambano dhidi ya Rushwa wenye kauli mbiu *"Kupambana na Rushwa ni jukumu langu".* TAKUKURU imeendelea na mapambano dhidi ya Rushwa kupitia sheria Mpya ya kuzuia na kupambana na Rushwa Na 11/2007 ambayo imeongeza wigo wa makosa ya Rushwa na jinsi ya kukabiliana nayo, katika sekta za Umma na binafsi. Wilaya ya Sumbawanga kwa kushirikiana na TAKUKURU imeendelea kutoa elimu kwa umma juu ya Rushwa na Madhara yake. TAKUKURU imefanikiwa kuendesha Semina kuhusu Rushwa, ambapo Mada 18 zilitolewa kwenye semina na Mikutano mbalimbali ya hadhara katika Kata za Halmashauri za Manispaa na Wilaya. TAKUKURU imefanikiwa kutembelea klabu 27 za wapinga rushwa katika Shule za Msingi na Sekondari, imewahamasisha Wanafunzi na wananchi kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa kufika ofisi ya TAKUKURU au kwa kutumia na kupiga namba ya bure 113. TAKUKURU inaendelea kupokea na kuchunguza taarifa za vitendo vya Rushwa, kukusanya ushahidi wa chunguzi mbalimbali, kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria watuhumiwa wanaobainika kutenda kosa kinyume na sheria Na 11/2017 ya kupambana na kuzuia Rushwa. Ushiriki wa Wananchi katika mapambano dhidi ya Rushwa umeongezeka ambapo katika kipindi cha Januari hadi Agosti, 2021 jumla ya malalamiko / tuhuma 84 zilipokelewa na malalamiko 15 yapo katika uchunguzi, na kesi 5 zilifikishwa mahakamani na zinaendelea kusikilizwa. Aidha katika kipindi cha Januari hadi Agosti, 2021 TAKUKURU kwa kushirikiana na Wilaya ya Sumbawanga imefanikiwa kuokoa shilingi za kitanzania 63,992,100/=, ambazo zilikuwa zitumike nje ya utaratibu wa utoaji wa huduma kwa Wananchi.

**Mheshimiwa Rais,** Ili kupunguza malalamiko kwa Wananchi juu ya Matumizi ya fedha za Serikali Wilaya imekuwa ikisisitiza uwazi katika matumizi ya fedha katika ofisi zake kwa kubandika taarifa za Mapato na Matumizi, kutokana na uwazi huu kiwango cha Wananchi kushiriki katika usimamizi na ufuatiliaji wa miradi umeongezeka.

### 2.1.2 Mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI

***Mheshimiwa Rais,*** Wilaya ya Sumbawanga inaendelea na mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI chini ya kaulimbiu isemayo "Mshikamano wa Kitaifa, Tuwajibike kwa Pamoja" kwa kutoa elimu juu ya kujikinga na maambukizi ya VVU na UKIMWI, kwa makundi mbalimbali katika jamii kwa njia ya semina, Vikao, Mikutano, Majarida na vitabu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama vile WALTEREED, PSI, ASCO, NACOPHA, PRO LICHIDE, THPS, SHDEPHA + Sumbawanga, MAUWARU na KONGA SUMBAWANGA. Makundi yaliyopatiwa elimu ni pamoja na vikundi 61 vya Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI venye jumla ya watu 1,452 wakiwemo wanaume 538 na wanawake 914. Wilaya ya Sumbawanga kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imeendelea kuwahudumia Watu 25,850 Wanaoishi na VVU wakiwemo wanaume 9,286 na wanawake 16,564. Aidha kati ya hao wanaotumia dawa za kufubaza makali ya Virusi Vya UKIMWI kutoka katika vituo vya kutolea huduma ni 19,975 ikiwa wanaume ni 13,287 na wanawake 6,688 sawa na asilimia 99.7%. Jumla ya watu 2,155 wakiwemo wanaume 708 na wanawake 1,447 wamejiunga katika vikundi wakishiriki shughuli mbali mbali za uzalishaji mali zinazowawezesha kupata mahitaji yao ikiwemo chakula bora. Takwimu zinazonyesha kundi kubwa lililoathirika zaidi ni la vijana na watu wenye umri kati ya miaka 15-49. Kiwango cha maambukizi kimeendelea kuwa 4.4 % hadi kufikia 2021. Kampeni dhidi ya Mapambano ya VVU na UKIMWI

zimefanyika kwa kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kupima VVU, kutoa huduma ya hiari ya Tohara kwa wanaume hadi kufikia Agosti 2021 jumla ya wanaume 10,262 wamepimwa na kufanyiwa Tohara. Huduma ya kupunguza maambukizi ya VVU kutoka kwa mama mjamzito kwenda kwa mtoto inaendelea kutolewa kwa lengo la kumkinga mtoto ambapo kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Agosti 2021 jumla ya kina mama 527 walipatiwa dawa kwa ajili ya kumkinga mtoto juu ya maambukizi. Vilevile Jamii inashauriwa kwenda kupima afya zao kwani kukutwa na maambukizi ya VVU si mwisho wa maisha. Hivyo napenda kuwasisitiza Wananchi tushirikiane kwa pamoja tuwajibike katika kulipunguza na hatimaye kulimaliza janga hili.

### 1.1.3 Mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya

**Mheshimiwa Rais,** Wilaya ya Sumbawanga imeendelea kukabiliana na tatizo la matumizi ya Madawa ya kulevya ambapo kwa kiasi kikubwa tunakabiliwa na tatizo la dawa ya kulevya aina ya Bangi ambapo kwa kipindi cha Januari hadi Agosti jumla ya Kg. 14.95 za bangi zilikamatwa. Katika kipindi hicho jumla ya Watuhumiwa 74 waliokamatwa kwa usambazaji wa Dawa za Kulevya, kati ya hao, kesi zilizoripotiwa zilikuwa 29 ambapo kati ya hizo 13 zilisajiliwa mahakamani, 16 ziko chini ya upelelezi na kesi 01 imefika mwisho na mtuhumiwa alifungwa . Ili kukabiliana na tatizo hilo Wilaya kwa kushirikiana na Wadau imeendelea kutoa elimu dhidi ya athari ya matumizi ya madawa ya kulevya ambapo waathirika ni vijana kuanzia miaka 18 na kuendelea. Jeshi la Polisi kwa kutumia kitengo cha polisi jamii kimekuwa kikitoa elimu kupitia njia ya redio (Chemchem, VOS na Ndingara), Vikundi mbalimbali kwa kutumia nyimbo, maigizo na ngonjela, elimu ya ana kwa ana katika Tarafa na Kata, Taasisi za Kidini, Mikutano ya hadhara. Makundi rika mbalimbali, CSO's, NGOs na FBOs yamekuwa yakishirikishwa katika kampeni za kupambana na Madawa ya kulevya. Katika kipindi cha Januari hadi Agosti Jumla ya Waathirika 5 wa Dawa za kulevya walibainika na kuwapeleka katika vituo vya afya ili kupata ushauri nasaha. Mikakati mbalimbali imekuwa ikitumika katika kuzuia kilimo, matumizi na biashara ya dawa za kulevya ikiwemo kuwachukulia hatua za kisheria kwa Wanaojihusisha. Kupitia kaulimbiu hii tunaendelea kutoa *Elimu sahihi juu ya Dawa za Kulevya na kuboresha huduma kwa Waraibu, Ewe Mwanachi chukua Hatua.*

### 1.1.4 Mapambano dhidi ya Malaria

***Mheshimiwa Rais,*** Ugonjwa wa Malaria ni miongoni mwa magonjwa yanayosumbua watu wengi katika Wilaya yetu. Kwa mujibu wa Takwimu za DHIS2 za Januari hadi Agosti, 2021 Watoto 56,096 wenye umri wa chini ya miaka 5 walihudhuria kwenye vituo vya kutolea huduma za afya. Kati ya hao watoto 11,721 sawa 20.9%, walikutwa na vimelea vya Malaria. Watu wazima 126,750 walifika kwenye vituo vya kutolea huduma. Kati yao watu 26,487 sawa na 20.9% walikutwa na vimelea vya Malaria. Wilaya imeendelea kushirikinana na Wadau kama vile 'Global Fund' na CHAI katika mapambano dhidi ya Maralia kwa kutoa Vyandarua, Usimamizi wa shughuli za Maralia na upatikanaji wa Takwimu sahihi za Maralia. Kwa ujumla kiwango cha maambukizi ya Malaria kinazidi kupungua mwaka hadi mwaka kutoka asilimia 29% Mwaka 2019 hadi asilimia 21% Mwaka 2020.

***Mheshimiwa Rais,*** Wilaya inaendelea na utoaji wa elimu ya kinga dhidi ya Malaria kwa jamii na kuelekeza matumizi sahihi ya vyandarua kila siku ambapo hadi kufikia Agosti 2020 jumla ya vyandarua 285,850 vyenye viwatilifu vyenye thamani ya shilingi 2,858,500,000 viligawiwa kwa

wananchi ambapo kila Chandarua kinagharimu Tsh. 10,000/=. Vyandarua hivi vilivyotolewa na Wizara ya Afya kitengo cha Malaria na kugawiwa kwenye vituo 83 vya kutolea huduma za Afya kwa ajili ya akina mama wajawazito na watoto chini ya miaka 5. Wilaya imeendelea na mikakati ya kutokomeza Malaria, kwa kuwasisitiza wananchi kufanya usafi wa Mazingira na kuondoa mazalia ya mbu sambamba na kupulizia dawa kwenye maeneo ya mazalia ya mbu. Kuhakikisha Akina Mama Wajawazito wanaofika Kliniki wanapata dawa za kuwakinga na malaria, ili kumkinga Mama mjamzito pamoja na Mtoto atakaye zaliwa asipatwe na Malaria. Kuhakikisha kuwa wote wanaobainika kuwa na maambukizi ya Malaria wanapata tiba. Hivyo basi kila Mwananchi achukue hatua ya kutokomeza Malaria *kwani "Ziro Malaria inaanza na Mimi-Chukua hatua kuitokomeza".*

### 1.1.5 Umuhimu na Uzingatiaji wa Lishe kwa Afya Imara

***Mheshimiwa Rais,*** Wilaya kwa kushirikiana na Wadau wa Lishe wameendelea kutoa elimu juu ya Lishe bora kupitia Mikutano ya Hadhara, Nyumba za Ibada, maadhimisho mbalimbali, vyombo vya habari na kupitia vituo 83 vya kutolea huduma za Afya. Hali ya Lishe Kimkoa na Wilaya zake ikiwemo Wilaya ya Sumbawanga imeboreshwa kutoka asilimia 56.3 % Mwaka 2014 hadi 47.9 % Mwaka, 2018 hii ni kutokana na ripoti ya Hali ya Lishe Tanzania (TNNS).
Hii inatokana na ufahamu wa Wananchi kuhusu umuhimu wa Lishe Bora, athari zitokanazo na Lishe duni na Madhara ya utapiamlo kwa ujumla.
Mikakati mingine ya kukabiliana na athari za lishe ni kuwepo kwa Kamati za Lishe za Wilaya, Kata, Vijiji na Mitaa, kupitia utekelezaji wa mradi wa Lishe Endelevu. Watoa huduma 442 ngazi ya Jamii wamejengewa uwezo wa namna ya kuwatambua Watoto wenye utapiamlo mkali ngazi ya Jamii. Aidha wazazi na walezi wa watoto wenye umri wa chini ya miaka 5 wamejengewa uwezo kupitia vituo vya kutolea huduma za afya ili kuwawezesha kutambua dalili mbalimbali za watoto wenye utapiamlo, ikiwa ni pamoja na matumizi ya kadi ya maendeleo ya Mtoto kila anapohudhuria Kliniki na kuchukua hatua stahiki ikiwemo kuwahi Kliniki mara wajitambuapo kuwa wajawazito.
Unasihi wa Lishe umefanyika kwa Wazazi/Walezi wenye Watoto chini ya miaka 5 kupitia vikundi Malezi ambavyo walengwa wake ni Wanawake Wajawazito, wanaonyonyesha na walezi wenye watoto wenye umri chini ya miaka 2. Kupitia vikundi malezi 1,543 mbali na unasihi, vimewezeshwa uzalishaji wa vyakula vyenye uwingi wa virutubishi kupitia mashamba darasa, wakijishughulisha na kilimo cha mbogmboga, matunda na ufugaji wa mifugo midogo midogo ili kuwezesha jamii kuweza kupata mlo kamili.

**Mheshimiwa Rais,** Ili kuhakikisha utekelezaji wa hafua za lishe unakuwa na ufanisi, mikakati ifuatayo imefanyia ikiwemo: - Kutenga bajeti ya kutekeleza afua za Lishe kwa kuzingatia idadi ya watoto chini ya miaka 5 waliopo. Bajeti imekuwa ikiongezeka kutoka Tsh. 97,605,100 mwaka 2018 hadi Tsh. 121,047,953.07 Mwaka, 2021. Mkakati pia ni kuendelea kuhamasisha jamii katika kilimo cha mbogamboga na matunda pamoja na ufugaji wa wanyama wadogowadogo kwa ajili ya kuliwa, kuwahimiza Wajawazito kuhakikisha wanahudhuria Kliniki mapema na kuhamasisha Akina Mama wenye Watoto chini ya miaka 5 kuhudhuria Kliniki kwa ajili ya kukamilisha huduma za chanjo kulingana na maelekezo ya Wizara ya Afya.

## 2.0 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA SEKTA MBALIMBALI

**Mheshimiwa Rais,** Katika kuhakikisha jamii inapata huduma bora Wilaya imeweza imefanikiwa katika nyanja mbalimbali ikiwemo Elimu ambapo ujenzi wa miundombinu ya madarasa kwa Elimu Msingi na Sekondari imeongezeka kutoka vyumba 1830 Mwaka 2019 hadi vyumba 1924 Mwaka, 2021, Maabara zimeongezeka Kutoka Maabara 30 Mwaka 2019 hadi 36 Mwaka, 2021, Matundu ya Vyoo kutoka 2810 Mwaka, 2019 hadi 2854 Mwaka 2021, Nyumba za Walimu zimeongezeka kutoka 1002 Mwaka 2019 hadi 1055 Mwaka 2021, Madawati yameongezeka kutoka 54675 Mwaka, 2019 hadi 68148 Mwaka, 2021. Mapokezi ya Fedha za Miradi ya Elimu yameongezeka kutoka Tsh. 2,604,861,668 Mwaka, 2019 hadi Tsh. 3,674,297,220 Mwaka, 2021 na fedha za Uendeshaji wa Shule (Capitation) imeongezeka kutoka Tsh. 2,633,751,763 Mwaka, 2019 hadi Tsh. 2,654,650,365 Mwaka 2021

**Mheshimiwa Rais,** Utoaji wa huduma umeendelea kuboreshwa kwa kuongeza miundombinu ya Afya kutoka Zahanati 75 Mwaka, 2019 hadi 78 Mwaka, 2021, Vituo vya Afya kutoka 7 Mwaka, 2019 hadi 10 Mwaka, 2021, Ujenzi wa Hospitali kutoka 0 Mwaka 2019 hadi 2 Mwaka 2021, Nyumba za Waganga kutoka 88 Mwaka 2019 hadi 89 Mwaka 2021, Upatikanaji wa dawa kutoka asilimia 87.35 Mwaka 2019 hadi asilimia 92.95 Mwaka 2021 na Mapokezi ya fedha za Miradi ya Afya yameongezeka kutoka Tsh. 1,703,000,000/= Mwaka, 2019 hadi Tsh. 3,397,683,918 Mwaka, 2021.

**Mheshimiwa Rais,** Huduma ya upatikanaji wa Maji safi na salama umeongezeka kutoka asilimia 86 Mwaka 2019 hadi asilimia 87 Mwaka, 2021 kwa Manispaa kutoka asilimia 71 Mwaka 2019 hadi asilimia 72 Mwaka, 2021 kwa Vijijini. Wilaya imeendelea kupokea fedha kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya Maji ambapo Mwaka 2019/20 zilipokelewa Tsh. 2,752,993,908/= na Mwaka 2020/21 zilipokelewa Tsh. 2,517,772,508.

**Mheshimiwa Rais,** Mtandao wa barabara umeongezeka mwaka hadi mwaka kutoka Kilomita za Lami 28.6 Mwaka 2019 hadi kilomita 29.3 Mwaka 2021. Aidha Wilaya imeendelea kupokea fedha kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya Barabara ambapo Mwaka 2019 zilipokelewa Tsh. 2,001,688,555 na Mwaka 2021 zilipokelewa Tsh. 1,942,850,005.

**Mheshimiwa Rais,** Wilaya kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali yakiwemo mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na ya Kidini imefanikiwa kutenga na kusimamia jumla ya Hekta 50,210.7 za hifadhi ya misitu. Kampeni za kuhamasisha uhifadhi na upandaji wa miti zimeendelea kufanyika. Kwa mwaka 2020/21 jumla ya miti 1,647,843 imepandwa katika maeneo mbalimbali ya Wilaya. Aidha doria mbalimbali ili kuhakikisha misitu inalindwa zimeendelea kufanyika.

**Mheshimiwa Rais,** Wilaya imeendelea kuweka msisitizo katika Kilimo ili kiwe na tija kwa kuhakikisha Wakulima wanatumia mbinu na zana za kisasa katika kilimo ambapo, katika msimu wa 2019/20 kumekuwa na ongezeo la mavuno kutoka tani 273,549.26 za Nafaka Mwaka, 2018/19 hadi tani. 369,351.92 Mwaka 2019/20 na Mazao jamii ya Kunde kutoka tani 60,401.9 Mwaka, 2018/19 hadi tani 64,669.85 Mwaka 2019/20 kuendelea kutumia. Aidha kuhakikisha

mifugo inakuwa na tija tumeendelea na uhamasishaji wa ufugaji wa kisasa ili kupata mazao ya mifugo yenye tija. Wilaya imeendelea kuhakikisha kuwa huduma za ugani zinapatikana.

**Mheshimiwa Rais**, Wilaya imeendelea kuhakikisha kuwa inatoa huduma bora kwa jamii. Mikakati mbalimbali imewekwa kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato, ikiwa ni pamoja na kusisitiza ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mfumo wa Kielektroniki (LGRCIS), kutokana na mikakati iliyowekwa makusanyo ya mapato yameongezeka kutoka Tsh. 5,059,227,669 Mwaka 2018/19 hadi Tsh. 5,448,593,156 Mwaka, 2020/21.

## 3.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI ILIYOPITIWA NA MWENGE WA UHURU 2019

***Mheshimiwa Rais,*** Katika mbio za Mwenge wa Uhuru wa Mwaka 2019, Mwenge wa Uhuru ulifanikiwa kupitia miradi 40, ambapo miradi 6 ilizinduliwa, Miradi 8 iliwekewa mawe ya Msingi, Kukaguliwa Miradi 9, Utoaji wa Mikopo kwa Vikundi 14 na Uhifadhi wa Mazingira Vikundi 3. Thamani ya miradi yote hiyo ilikuwa ni Shilingi 14,496,377,552.43, kati ya kiasi hicho Halmashauri zilichangia Shilingi 608,364,106/- Serikali kuu Shilingi 13,141,683,646/-, Wananchi Shilingi 176,410,000.43/- na Wadau wengine wa Maendeleo Shilingi 574,919,800/-.

## 4.0 MIRADI ILIYO ZINDULIWA, KUKAGULIWA, KUTEMBELEWA NA KUWEKEWA MAWE YA MSINGI, MWAKA 2021.

***Mheshimiwa Rais*,** Katika mbio maalumu za Mwenge wa Uhuru wa Mwaka, 2021, Mwenge wa Uhuru Umekimbizwa na kupita katika vijiji 15 katika umbali wa Km 120. Hadi kukabidhi utatumia umbali wa Km.152. Mwenge umefanikiwa kupitia miradi 10 kwa kuzindua, kuweka mawe ya Msingi na Kukagua. Kati ya hiyo Elimu 2, Maliasili 1, TEHAMA 1, Utoaji Mikopo 2, Afya 2, Mradi wa Umeme 1 na Barabara 1. Thamani ya miradi yote ni shilingi 8,753,603,292/-, kati ya kiasi hicho Serikali kuu imetoa Shilingi 8,632,087,292/-, Wilaya imechangia Shilingi 104,466,000/-, Wananchi wamechangia Shilingi 2,250,000/- na Wadau wengine wa Maendeleo Shilingi 14,800,000/-.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU UBARIKI MKOA WA RUKWA, MUNGU IBARIKI WILAYA YA SUMBAWANGA.**

**MWENGE WA UHURU 2021 OYEEEEEEE!!!!!!!!!!!!!**

**Imeandaliwa na kuthibitishwa na:**

**JINA:** MHE. SEBASTIAN WARYUBA

**WADHIFA:** MKUU WA WILAYA YA SUMBAWANGA

**SAINI / MUHURI. . . . . . . . . . . . . . . . ....**

**TAREHE: 20/09/2021**.